# OFISI YA WAKIMBIZI YA JIMBO LA NORTH CAROLINA
# MPANGO WA KUJITOSHELEZA KWA FAMILIA (DSS-6230) SEHEMU YA B

Jina la Mteja:
Nambari ya Mgeni: Ukubwa wa Mpango:

| | | | |
|---|---|---|---|
| MAPATO YA KILA MWEZI | Mapato ya 1 | | $ |
| | Mapato ya 2 | | $ |
| | Mapato ya 3 | | $ |
| | Mapato ya 4 | | $ |
| | **Mapato ya Jumla kwa Mwezi:** | | **$** |
| MANUFAA YA KILA MWEZI | Msaada wa Fedha | (RCA, TANF, MG, SSI, nk.) | $ |
| | SNAP | | $ |
| | Manufaa Mengine | (WIC, SSDI, n.k.) | $ |
| | Mengine | | $ |
| | **Jumla ya Manufaa ya Kila Mwezi:** | | **$** |
| GHARAMA ZA KILA MWEZI | Kodi ya Nyumba/ Mkopo wa Nyumba | | $ |
| | Gesi | | $ |
| | Umeme | | $ |
| | Maji | | $ |
| | Muunganisho wa Mtandao/Intaneti | | $ |
| | Simu | | $ |
| | Vyakula | | $ |
| | Usafi wa Mwili | (sabuni, dawa ya kusafisha n.k.) | $ |
| | Usafiri | (basi, malipo ya gari, bima, n.k.) | $ |
| | Mkopo wa Kusafiri | | $ |
| | Bima | (afya, magari, wapangaji, n.k.) | $ |
| | Akiba | | $ |
| | Mengine | | $ |
| | Mengine | | S |
| | Mengine | | $ |
| | Mengine | | $ |
| | **Jumla ya Gharama za Kila Mwezi:** | | **$** |
| Makadirio ya Mapato ya Jumla | (Jumla ya Mapato + Jumla ya Manufaa) – Jumla ya Gharama = **Makadirio ya Mapato ya Jumla ya Familia** | | |

Kulingana na mshahara wa wastani kwa mwezi na gharama ya maisha katika jiji lako, hali hii kwa sasa inachukuliwa kuwa ya kujitosheleza?

☐NDIYO ☐HAPANA

Ikiwa hapana, tafadhali jaza mpango/mipango ya uwezo wa kuajiriwa kwa ___________________________________

Ikiwa ndiyo, tafadhali toa sababu kuu ya kujiandikisha katika huduma (yaani, kujifunza ujuzi upya, kupanda daraja la kazi, haja ya huduma zingine za ajira, n.k.): ____________________________________________________________

Mfanyakazi ____________________________________________________________

Jina Saini Tarehe

OFISI YA WAKIMBIZI YA JIMBO LA NORTH CAROLINA
MPANGO WA KUJITOSHELEZA KWA FAMILIA (DSS-6230) SEHEMU YA B

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mteja | | | |
| | Jina | Saini | Tarehe |
| Mkalimani | | | |
| | Jina | Saini | Tarehe |

## MAELEKEZO:

Madhumuni ya fomu hii ni kutoa njia ambayo mtoa huduma ya wakimbizi anaweza kumsaidia mteja katika kuamua kiasi cha mapato ambayo yatahitajika ili mteja aweze kujitegemea kiuchumi, na kiasi cha rasilimali ambazo zitapatikana kwa mteja kama anapopiga hatua za kuweza kujitegemea kiuchumi. Mfanyakazi wa Shirika lazima ajaze fomu hii kabla ya kutolewa kwa huduma. Fomu hii inapaswa kujazwa kwa kila mteja/familia ambao inapokea huduma za ajira. Ikiwa huduma za ajira zinatolewa kwa wanafamilia wengi ambao gharama zao ni sawa, bajeti kamili lazima ijazwe na mkuu wa familia, lakini nakala ya fomu iliyojazwa/zilizojazwa inaweza kuwekwa kwenye faili za wanafamilia wanaofuata.

| | |
|---|---|
| Jina la Mteja: | Andika jina la mtu unayemuundia mpango huo. |
| Nambari ya Mgeni: | Jumuisha Nambari ya Mgeni ya mteja ambaye unamuundia mpango. |
| Ukubwa wa Mpango: | Onyesha idadi ya washiriki waliojumuishwa kwenye mpango kama ilivyobainishwa kwenye fomu ya DSS-6230 Sehemu ya A. Hii inaweza kujumuisha wategemezi au mtu mwingine yeyote ambaye anamtegemea mteja kifedha. |

**MAKADIRIO YA MAPATO YA KILA MWEZI:**

Kadiria mshahara wa kila mwezi ambao kila mtu mzima anayeweza kuajiriwa hupata katika familia katika nafasi zilizowekwa. Hii inaweza pia kujumuisha mapato ya ajira ya binafsi, kama vile mapato ya ziada ambayo familia inapata kupitia biashara ya kibinafsi (ususi, huduma ya utunzaji wa watoto mchana nyumbani, n.k.). Ongeza jumla ya kiasi ili kubaini Jumla ya Mapato ya Kila Mwezi.

**MAKADIRIO YA MANUFAA YA KILA MWEZI:**

Kadiria jumla ya mapato ya manufaa ya kila mwezi ambayo familia inastahili kupata kwenye visanduku vya aina manufaa. Ongeza jumla ya kiasi ili kubaini Jumla ya Mapato ya Manufaa ya Kila Mwezi.

| | |
|---|---|
| Msaada wa Fedha: | Inaweza kujumuisha RCA, TANF, SSI, nk. |
| SNAP: | Ikiwa mteja/familia inapokea msaada wa SNAP, unaojulikana pia kama vocha za chakula, onyesha kiasi cha kila mwezi. |
| Manufaa Mengine: | Tafadhali onyesha ikiwa mteja/familia inapokea aina nyingine yoyote ya msaada, kama vile WIC, SSDI, n.k. |

**MAKADIRIO YA GHARAMA ZA KILA MWEZI**:

Kadiria jumla ya gharama za kila mwezi za mteja/familia. Ikiwa wanagawana gharama, kwa mfano na mtu anayeishi naye katika chumba kimoja, onyesha kiasi ambacho mteja anapaswa kulipa. Ni sawa kukadiria iwapo mteja hana uhakika kuhusu kiasi kamili. Ikiwa mteja au familia haiwajibiki/haina gharama fulani, tafadhali andika "Haitumiki" Ongeza jumla ya kiasi ili kubaini Jumla ya Gharama za Kila Mwezi.

| | |
|---|---|
| Kodi ya Nyumba/<br>Mkopo wa Nyumba: | Jumuisha kiasi cha kodi ya nyumba ambacho familia inapaswa kulipa kila mwezi. |
| Gesi/Mafuta: | Jumuisha kiasi kinachokadiriwa ambacho mteja atalipa kwa huduma ya gesi/mafuta kila mwezi. |
| Umeme: | Jumuisha kiasi kinachokadiriwa ambacho mteja atalipa kwa huduma ya umeme kila mwezi. |

OFISI YA WAKIMBIZI YA JIMBO LA NORTH CAROLINA
MPANGO WA KUJITOSHELEZA KWA FAMILIA (DSS-6230) SEHEMU YA B

| | |
|---|---|
| Maji: | Jumuisha kiasi kinachokadiriwa (ikiwa kipo) ambacho mteja atalipa kwa huduma ya maji kila mwezi. |
| Muunganisho wa Mtandao/Intaneti: | Jumuisha kiasi kinachokadiriwa (ikiwa kipo) ambacho mteja atalipa kwa huduma ya muunganisho ya mtandao na/au intaneti kila mwezi. |
| Simu: | Jumuisha kiasi kinachokadiriwa ambacho mteja atalipa kwa huduma za simu kila mwezi. |
| Chakula: | Kadiria kiasi ambacho mteja/familia italipa kwa chakula kila mwezi. |
| Usafi wa Mwili: | Kadiria kiasi ambacho mteja/familia italipa kwa bidhaa za usafi wa mwili kama vile sabuni, losheni, nk, kila mwezi. |
| Usafiri: | Kadiria kiasi ambacho mteja/familia itahitaji kwa usafiri kila mwezi. Ikiwa mteja/wateja watatumia mfumo wa basi la umma, jumuisha gharama inayokadiriwa ya nauli za basi. Ikiwa mteja/wateja watatumia usafiri wa pamoja, jumuisha kiasi ambacho kila mtu katika familia atalipa kila mwezi kwa usafiri wa pamoja kwenda mahali wanakoenda. Ikiwa mteja/wateja wana gari, jumuisha gharama inayokadiriwa ya mafuta ya gari ya kila mwezi, ada ya leseni na ukaguzi na gharama za ukarabati unaotarajiwa. |
| Mkopo wa Kusafiri: | Jumuisha kiasi cha mkopo wowote wa kusafiri ambao haujalipwa ambao familia inapaswa kulipa kwa gharama zao za kusafiri. Jumuisha malipo ya mkopo ya kila mwanafamilia. |
| Bima: | Kadiria kiasi ambacho mteja/familia itahitaji kulipa kwa aina zozote za bima inayoweza kuzihitaji. Mifano inaweza kuwa ni pamoja na: Bima ya Afya, Bima ya Mwenye Nyumba au Wapangaji, Bima ya Gari, n.k. |
| Akiba: | Kukadiria kiasi ambacho mteja / nyumba anataka kuokoa kila mwezi. |
| Nyingine: | Kwa kuwa hali ya kila mteja ni tofauti, kuna mistari kadhaa ya kuweka gharama za ziada ambazo haziwezi kujumuishwa kwa kategoria zingine. Ikiwa inafaa, tafadhali andika aina ya gharama na makadirio ya kila mwezi kwa kila moja katika mistari iliyowekwa. Mifano inaweza kujumuisha: |
| Huduma ya Matunzo ya Watoto: | Kadiria kiasi (ikiwa ipo) ambacho mteja atalipa kwa huduma ya matunzo ya watoto kila mwezi. |
| Nguo: | Kadiria kiasi ambacho mteja atalipa kwa mahitaji ya nguo kila mwezi. |
| Elimu: | Kadiria kiasi ambacho mteja/familia angependa kutenga kila mwezi kwa gharama za elimu. |

**MAKADIRIO YA MAPATO YA JUMLA**:
Piga hesabu ya tofauti kati ya Mapato (mapato + manufaa) na Gharama ili kukadiria mapato ya jumla ya mteja/familia. Kwa kutumia kiasi hiki, pamoja na mishahara ya wastani na gharama ya wastani ya maisha katika eneo lako, hali hii kwa sasa inachukuliwa kuwa ya kujitosheleza? Tafadhali onyesha ndiyo au hapana.

Ikiwa hapana, tafadhali onyesha ni nani katika hali hiyo utakayemjazia mpango wa uwezo wa kuajiriwa (DSS-6232). Ikiwa ndiyo, tafadhali toa sababu fupi ya kumwandikisha mteja katika mpango wa uwezo wa kuajiriwa (DSS-6232). Sababu zinaweza kuwa ni pamoja na kupanda daraja la kazi, kujifunza ujuzi upya/uthibitishaji, n.k.

| | |
|---|---|
| Mfanyakazi wa Shirika: | Fomu hiyo inapaswa kuwa na saini na tarehe ya ambayo Mfanyakazi wa Shirika alijaza Mpango wa Kujitosheleza kwa Familia na mteja. |
| Mteja: | Fomu hii inapaswa kuwa na saini na tarehe ya mteja, inayoonyesha kwamba ameona, ameelewa na anakubali Mpango wa Kujitosheleza wa Familia uliojazwa kama ilivyobainishwa. |

OFISI YA WAKIMBIZI YA JIMBO LA NORTH CAROLINA
MPANGO WA KUJITOSHELEZA KWA FAMILIA (DSS-6230) SEHEMU YA B

Mkalimani: Fomu hii inapaswa kuwa na saini na tarehe ya Mkalimani. Ikiwa hakuna mkalimani aliyehitajika, tafadhali onyesha “Haitumiki”

**Fomu hii inapaswa kujazwa kwa pamoja na**
**Mpango wa Mafunzo ya Ufundi (DSS-6228) na/au Mpango wa Uwezo wa Kuajiriwa (DSS-6232)**
**na Mfanyakazi wa Shirika.**